Ecolebooks.com

***P320/1***
***KISWAHILI***
***Paper 1***
***July 2019***
*3 Hours*

# MOCK EXAMINATIONS 2019

***Uganda Advanced Certification of Education***

**MITIHANI YA MWIGO**

**FASIHI YA KISWAHILI P320/1**

**Karatasi ya Kwanza**

MUDA: Saa Tatu

**(***UFAHAMU, NATHARI NA USHAIRI)*

**MAAGIZO:**

a) *Jibu maswali* ***matatu.***
b) *Chagua swali moja kutoka kila sehemu, yaani* ***A, B na CH.***
c) *Usijibu swali zaidi ya moja kutoka diwani moja wala maswali mawili kutoka sehemu ya* ***CH****.*
d) *Nadhifisha mwandiko wako.*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

## SEHEMU A: UFAHAMU *(alama 33)*

1. ***Soma taarifa ya habari ifuatayo kasha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini yake:***

Nchi takribani zote za kiafrika hutegemea kilimo. Ni dhahiri shahiri kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa sisi watu weusi. Kwa miaka mingi sana imejulikana kuwa uchumi wa nchi unakuzwa Zaidi na wakulima wetu mashambani. Kwa asilimia kubwa, wanawake ndio wanaojitoa muhanga na kufanya mambo mengi kutwa nzima. Kwa kuwa mfumo wao wa kufanya kazi ni huohuo siku nenda, siku rudi, matokeo ya juhudi zao huwa ni ya kadiri tu, lakini ni yenye kunufaisha nchi nzima.

Hebu tumwangalie mwanamke wa wastani katika jamii ya kawaida ya mwanafrika pamoja na shughuli zake za siku nzima na hata kwa mwezi na mwaka. Mwanamke hufanya kazi wakati wote. Kila uchao huwa mbioni akijitahidi kutekeleza majukumu yake. Kazi za mwanamke zinakadiriwa kuchukua saa kama kumi na sita kila siku hata akilala usiku ni kujibwaga tu kitandani kama mzigo mzito. Jambo la kushangaza ni kwamba mwanamke huyo hanung'unikii hali hii na kushindana na wanaume bali huichukulia kama ni wajibu wake. Tangu jadi, nyanya zetu huamini kuwa ni majaliwa yao kutekeleza huduma na kazi mbalimbali mithili ya punda. Kwa hivyo, wanawake hutenda shughuli zao karibu zote kwa hiari na mapenzi yao. Wao hunuia kufanya kazi vizuri zaidi na zaidi kila wakati na kwa hivyo huzalisha mali zaidi.

Wengi wa akina mama hawa hudamka saa kumi na moja alfajiri kutengeneza kiamsha kinywa au kupasha moto kiporo, kunadhifisha viunga vyao, kukama ng'ombe (Kama wanao) na kutayarisha mifugo tayari kwa mchungaji kuipeleka malishoni. kama mifugo si ya Kupelekwa malishoni, kina mama hao hutafuta majani ya mifugo hiyo. Baada ya shughuli hizi, wao huenda shambani ambapo hulima na kupanda au kupalilia na kuvuna. Baada ya kujiona wamechoka kulima, huenda kutafuta kitu cha kurudi nacho nyumbani. Huenda kuchuma mboga za majani au kutafuta vijikuni au kubeba chochote walichovuna. Mabwana wengine huwa shambani pamoja na wake zao, lakini hawahusiki sana katika kazi hizo za kubeba kuni au kutafuta mboga.

Wanawake wanaporudi kutoka kondeni kama hawani maji huenda kuteka maji. Aghalabu huwabidi kwenda mbali kuteka maji, maana vijijini hakuna mifereji ya mabomba na visima, mabwawa, maziwa na mito iko mbali na vijiji. Wakishapata maji

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

hupika na baada ya kula chakulahuendawakafikiria habari ya kufua nguo,na kishja kutengengeneza chajio,yaani chakula cha jioni. Kama kuna kuuza maziwa na bidhaa nyingine mwanamke huyu atapanga ya mauzo.

Kichwa cha mama huyu huzalisha mambo mengi ya kukuza uchumi. Kila watembeapo utawaona kila wakati wamo mbioni wakifanya mambo ya kujiinua kiuchumi.

Hebu mchunguze mama anayerudi kutoka shambanina mgongoni huenda akawa amebeba mtoto pamoja na kiondo kilichojaa chakula na pengine ni mja-mizito anashona sweta la mtoto au mumewe; akilini aanafikiriya jinsi atakavyolisha familia yake. Wanawake wa aina hii hutaenda kazi mithili ya mchwa. Hawachoki na kila siku huwa kiguu na njia kufanya kazi wazipatazo na wazimuduzo. Kama mtu mjuzi wa uchumi akipiga hesabu ya kazi na pesa zina zotokana na juhudi hizi ataona huenda wanawake hao hufanya kazi zinazoiniza shilingi 500 kwa siku.

Katika hali kama hii hatuna budi kuona kwamba wanawake huelemewa na mizigo mikubwa mikubwa na hatimaye kunyonya damu na nguvu zao na kuifuja miili yao na kuzeeka haraka haraka.

Tukikumbuka umuhimu wa wanawake katika jamii, mbali na ule wa kuwa wabeba mimba. Wazazi na walezi wa watoto wetu, mwanamke ni mwenzi na msuhuba kwa mwanamume na ni sehemu muhimu ya nguvu-kazi inayoaminika katika kuleta na kukuza maendeleo ya jamii zetu. Pia tusisahau wingi wao mbali na uhodari , juhudi na maarifa waliyo nayo. Katika hali kama hii taifa lolote lile jukumu Kubwa sana la kukumbuka, kuheshimu na kulinda kazi za wanawake kuishi kibinadamu.

Ili kufikia lengo hili haitoshi kuzungumza na koropoka kwenye vyombo vya habari, linalohitajika ni kuelimishaumma; kike kwa kiume. Waelimishwe wanawake kwa sababu wengi wamelemaa na kuvia kudhani kwamba halizao ni hali za majaaliwa na kwamba yote magumu watendayo ni wajibu kwao pia ipo haja ya kuwaelimisha wanaume – wanaume waelimishwe kujua kipimo cha usumbufu wa mwanamke; Na si kipimo cha usumbufu wao tu, bali kipimo cha utu, usuhuba na wapenzi wao na kisha wajibu wa pande mbili; kiukeni na kuumeni. Wanaume wengi hawatambui hayo, wanahisi kwamba nafasi ya mwanamke katika jamii ni kuzaa na kujukuu, kupika na kupakua, kufua na kupiga pasi, kusafisha na kufuta , kulima na kuvuna – bas! Pengine heshima anayopewa mwanamke ni ile ya ni ile ya kutekwa kisaikolojia; yaani ya kusifiwa kiuzuri, kimavazi na kulindwa kwa wivu na uchungu. Wakati utakapofika ambapo wanawake na wanaume

watakuwa wameelimishwa na kuelimika ndipo kila upande utakapofahamu wajibu na upasao wa kuishi kimasikilizano, mshikamano na maendeleo mengi yatapatikana humu nchini na kote barani Afrika.

**Maswali**

(a) Kulingana na taarifa hii, ni kwa nini kilimo ndicho uti wa mgongo wa nchi nyingi za kiafrika? (*alama 4)*

(b) Eleza mambo yanayomkabili mwanamke katika hali ya usumbufu. *(alama 6)*

(c) Mwandishi anatoa mapendekezo yapi ili kutatua shida za mwanamke? *(alama 6)*

(d) Kwa mujibu wa taarifa hii, Wanaume wana mitazamo ipi juu ya wanawake? (*alama 6)*

(e) Kuhingana nataarifa hii, wanawake katika jamii zetu hutoa huduma zipi? (*alama 5)*

(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. (*alama 6)*

(i) Kutenda kazi mithili ya punda.

(ii) kujitoa mhanga.

(iii) kilimo ni uti wa mgongo.

## SEHEMU B: NATHARI

***2. Soma chopoleo ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini:***

Hapo zamani za kale, baada ya kuumbwa ulimwengu na vyote vilivyomo ndani mwake, Mungu alifikiria sana juu ya uhai wa binadamu. Akawa anatatizika katika kuamua iwapo wanandamu wangeishi milele na milele bila kufa kama yeye, au wafe baada ya kuishi ulimwengu kwa muda. Hatimaye, akawatuma wajumbe wawili kuwaambia wanadamu wafanye uamuzi wao wenyewe kuhusu jambo hilo. Kwanza, akamtuma Kinyonga na kumpa ujumbe huu: "Mmeambiwa msizaane. Mbaki nyinyi wawili tu ulimwenguni: mke na mume, msife milele na milele."

Kinyonga akaupokea ujumbe na kuelekea ardhini. Kisha Mungu, nyuma yake, akamtuma Njiwa na ujumbe huu: "Mmeambiwa, mkitaka mzaane, kisha mfe. Mkifa, uhai utaendelezwa na

Ecolebooks.com

watoto, wajukuu, vitukuu, vilembwe na vilembwekeza wenu. Kwa jinsi hivyo, ijapokuwa ninyi wenyewe mtakufa, uhai hautaisha duniani. Utadumishwa na hao mtakaowazaa na watakaozaliwa nao. Ninyi mtakumbukwa milele na milele"

Kinyonga, kama itakavyokumbukwa alitumwa yeye mbele. Lakini kwa sababu ya mwendo wake wa mbele na nyuma, akafika wakati sawasawa na Njiwa. Akaanza kutoa ujumbe wake ambao, japo ulikuwa mfupi, hakuuwasilisha kwa haraka kwa sababu jambo la kwanza, yeye aligugumiza. Tena, alirudiarudia maneno kiasi cha kuchosha. Hivyo basi, wanadamu walipoona Kinyonga anachelewa kuuwasilisha kwa haraka ujumbe wa Mungu, wakamkemea kwa kumcheka. Kisha wakamwabia Njiwa atoe ujumbe wake kabla ya kinyonga kufanikiwa kufanya hivyo. Chapuchapu, njiwa akatoa ujumbe wake, japo ulikuwa mrefu. Wakausikiliza kwa makini. Wakaona ni ujumbe mzuri, wakaukubali.

Walipoukubali tu, Kinyonga naye akahitimisha kuwasilisha ujumbe wake. Huo wakauona mzuri zaidi, na hivyo wakataka kubadilisha uamuzi wao. Hapo, sauti ya Mungu ikasikika ikisema kwamba kubadilishwa hakuwezekani; tayari alikuwa amekwishapokea uamuzi wa na akaukubali. Walipotaka kuuliza maswali, sauti hiyo ikatoweka ghafla. Ikawa sasa ni kujilaumu wenyewe na kuwalaumu wale wajumbe wawili, hasa kinyonga, kwa kigugumizi chake na mwendo wake wa polepole. hata hivyo, lawama zao hazikufua dafu. Kikomo chao kikawa kimeshafungwa. Wakawa hawana budi kuzaana na kufa.

**Maswali:**

a) Hadithi hii ni ya aina gani? Toa ithibati ya jibu lako. *(Alama 03)*

b) Kwa mujibu wa hadithi nzima, eleza sifa za mhusika kinyonga. *(Alama 04)*

c) Taja na ulezee mbinu za kisanaa zinazopatikana kwenye habari hii. *(Alama 06)*

d) Fafanua muundo wa habari hiyo. *(Alama 06)*

e) Chambua mtindo wa habari kama ulivyobainishwa na mwandishi. *(Alama 06)*

f) Tamathali ya semi ya *Tashihisi* imejitokezaje katika habari hiyo? Eleza kwa kutoa Mifano thabiti. *(Alama 03)*

g) Mwandishi amegusia maudhui gani humo hadithini? Eleza *(Alama 05)*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

## SEHEMU CH: USHAIRI

**Sauti ya Dhiki:** Abdalatif Abdallah

**Ama**

3. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;*

**LIPI LITAKALOKUWA?**

Lipi mojapo kuwa? Naliwe lijilikane
Liwe tupate lijuwa, tujuwe na tulione
Naliwe tupate tuwa, liwapo ndilo tunene
Halitakuwa jingine, ima ndilo au silo

Naliwe lijitokeze, bure lisifitamane
Kama ni nuru ingaze, ingarishe pembe n'ne
Ni giza? Lifunikize, kila mbele tusione
Halitakuwa jingine , ima ndilo au silo

Li situndundishe nyoyo, naliwe nazo zisone
Tangu hapo wayowayo, na nyonyo liembetene
Yatosha ziliyonayo, lisizitweke mingine
Halitakuwa jingine, ima ndilo au silo

Kama lataka naliwe, hakika ijulikana
Bure lisitusumbuwe, kwanini tusumbuwane?
Lisipottaka lisiwe, wala tusiraiyane
Halitakuwa jingine, ima ndilo au silo.

***Maswali:***

a) Ukirejelea shairi hili, fafanua aina ya ushairi na aina ya shairi. *(Alama 04)*

b) Kwa kutoa ushahidi kutoka kwenye shairi lenyewe, fafanua umbo la shairi hili. *(Alama 08)*

c) Malenga ametumia toni gani katika shairi hilo? Fafanua. *(Alama 02)*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

d) ukirejelea shairi hili, thibitisha kwa kutumia mifano kwamba shairi hili linazingatia *ushairi wa arudhi.* *(Alama 10)*

e) Kwa kurejelea shairi hilo, taja na uelezee bahari zilizomo - *(Alama 08)*

f) Eleza dhamira inayopatikana katika shairi hilo. *(Alama 02)*

**Au**

***4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;***

1. Tumishi inuka hima, utwae wangu waraka
Huko nitakokutuma, uwenende kwa haraka
Na haya mate natema, hima yasije kauka
Inuka sasa inuka
2. Nenda kwa mwenzangu mja, kanisalimiye sana
Mwambe ni zetu pamoja, huzuni anazoona
Mambo hwenenda yakija, ni dasituri bayana
’kipeleleze ’taona
3. Nasivundikwe na moyo, kwa mambo yalotuswibu
Sisi kufikwa na hayo, si kitu kilo ajabu
Tushike tuliyonayo, tusiyawate swahibu
Nyoyo zisife kwa tabu
4. Kama hayo ’mewafika, waliwoanza azali
Walokuwa wakitaka, haki ishinde batwili
Walifikwa na mashaka, sampuli sampuli
Nasi tusitahamali

**Maswali:**

(a) Unadhani ni kwanini shairi hili liitwe msuko?. *(Alama 04)*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

(b) Eleza jinsi mshairi alivyotumia lugha katika shairi lake. *(Alama 10)*

Ch) Chambua bahari zinazopatikana katika shairi. *(Alama 10)*

(d) Fafanua vipengele vifuatavyo ukirejelea shairi hili;

i) Vina ii) Mizani *(Alama 04)*

(e) wewe kama msomaji wa shairi hili, unapata mafunzo gani? *(Alama 06)*

**Malenga wa Mrima:** Mwinyi Hatibu Mohamed

***Ama***

5. *Soma shairi lifuatalo kutoka diwani ya Malenga wa Mrima: Mwinyi Hatibu Mohamed kisha ujibu maswali yaloulizwa.*

**DUNIA NJIA PANDA**.

Dunia njia ya panda, kama nyinyi hamnazo
Aendaye akienda , siende mfululizo
Waume imewashinda, tokea zamani hizo
Dunia njia ya panda, hukanganya wasafiri

Endaye moja kwa moja, kwa pupa na chapukizo
Njia pasi kuzichuja, kwa pole na matulizo
Hapati punje ya tija, ila tama na vikwazo
Dunia njia ya panda, hukanganya wasafiri

Njia panda danganyifu, ilaye ni vibengezo
Hukanganya wasanifu, kwa shaka na mapotezo
Wakaukasa wokoju, manusura na pumbazo
Dunia njia ya panda, hukanganya wasafiri

Moja ni ya kivulini, na pambo za mjaazo
Ya pili ni njia duni, shimo la mateketezo
Yataka tuzibaini, twepukane na mizozo
Dunia njia ya panda, hukanganya wasafiri

Njia panda hupoteza, mwanzoni na mwishilizo
Ikatia mtu giza, la fahamu na mawazo

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Laiti mwaichunguza, mamboye ni msangazo
Dunia njia ya panda, hukanganya wasafiri

Na sisi binadamu, si mno mapatilizo
Tumekuliwa na hamu, sahau na mapuuzo
Ile imwagayo damu, ndilo letu pendekezo
Dunia njia ya panda, hukanganya wasafiri

Ingawa kwa hivi sasa, hakukosi vielezo
Na marubani huasa, kwa kemi na matangazo
Hatushiki twajitosa, tukaacha maagizo
Dunia njia ya panda, hukanganya wasafiri

**Maswali:**

(a) Unadhani Shairi hili limebeba bahari gani? *(Alama 08)*

(b) Eleza jinsi mshairi alivyotumia lugha katika shairi lake. *(Alama 08)*

Ch) Eleza maudhui angalau manne yanayopatikana katika shairi. *(Alama 08)*

(d) Andika ubeti wa **4** katika lugha nathari. *(Alama 04)*

(e) unafikiri ni kwanini shairi hili liitwe Tarbia? Fafanua. *(Alama 02)*

(f) wewe kama msomaji wa shairi hili, unapata mafunzo gani? *(Alama 06)*

**Au**

6. Diwani ya Malenga wa Mrima na Mwinyi Hatibu Mohamed, imekusanya tungo za mashairi yenye maadili tele. Kwa kutoa ushahidi kitabuni tathmini ukweli wa madai hayo. *(Alama 34)*

***MWISHO***

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**